



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA

Simu: +255262965679, +255262965676, +255622225618
Barua pepe: ded@kaliuadc.go.tz
Tovuti: www.kaliuadc.go.tz

S. L. P 83
Kaliua Tabora

KDC/M.Z/VOL.III/0056/03

23/09/2020

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MSAIDIZI WA HESABU
DARAJA LA II NA MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua anawatangazia Wananchi wote wenye sifa kuomba nafasi za kazi ya Msaidizi wa Hesabu Daraja la II na Mtendaji wa Kijiji Daraja la III kwa wote wenye sifa kama ifuatavyo:-

A: MSAIDIZI WA HESABU DARAJA LA II (NAFASI 1)

1. Sifa za Mwombaji

- i. Awe na Elimu ya Kidato cha nne (Form Four) au Sita (Form Six)
- ii. Kuajiriwa wenye cheti cha Astashahada ya Uhasibu kutoka Chuo kinachotambulika na Serikali au Acheti cha ATEC kinachotolewa na NBAA au sifa nyingine zinazolingana na hizo zinazotambulika na NBAA

2. Kazi za kufanya

- i. Kuandika na kutunza "register" zinazohusu shughuli za Uhasibu.
- ii. Kutunza kumbukumbu za hesabu
- iii. Kupeleka barua/nyaraka za Uhasibu Benki
- iv. Kufanya kazi nyingine za fani yake atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi.

B: MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III (NAFASI 1)

1. Sifa za Mwombaji

Awe na Elimu ya Kidato cha nne (Form Four) au Sita (Form Six) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti (NTA LEVEL 5) katika moja ya fani Zifuatazo:- Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na

Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

2. Kazi za kufanya

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya kijiji
- ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa amani na msimamizi wa Utawala Bora katika kijiji
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kijiji
- iv. Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya kijiji
- v. Kutafsiri na kusimamia Sera, sheria na Taratibu
- vi. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali
- vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaalamu katika Kijiji
- viii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji
- ix. Mwenyekiti wa kikao cha wataalamu waliopo katika kijiji
- x. Kupokea, kusikiliza na kutatua migogoro ya wananchi
- xi. Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za kijiji
- xii. Kusimamia ukusanyaji wa mapato katika kijiji
- xiii. Kuandaa na kutunza rejista ya Wakazi wote wa kijiji
- xiv. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata

3. MASHARTI YA JUMLA

- i. Mwombaji awe raia wa Tanzania
- ii. Mwombaji awe na umri usiozidi miaka 45 na awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
- iii. Maombi yote yaambatanishwe na maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV).
- iv. Maombi yote yaambatanishwe na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya elimu (IV au VI), cheti cha kuzaliwa na picha mbili za rangi za hivi karibuni (passport size) Ziandikwe jina la mwombaji nyuma.
- v. Testimonials Provisional results "Statement of results" hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita HAVITAKUBALIWA.
- vi. Waombaji watakaowasilisha taarifa na sifa za kughushi watachukuliwa hatua za Kisheria.

4. Maombi yatumwe kwa:-

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA,
S.L.P.83,
KALIUA.

Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni tarehe 07/10/2020 saa 9.30 mchana.


J. D. Mwaga

Mkurugenzi Mtendaji Wilaya

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA KALIUA
S.L.P. 83
KALIUA